

**Mwanafunzi: Irene Maundu**

Mwalimu: John Mwangi

Shule: Lukenya Academy

***(Maliza hivi)...tangu siku hiyo, maisha yangu yalichukua mkondo mpya.***

TAMAA MBELE MAUTI NYUMA

Naam, jua liliaga miti na nuru ya mchana ikafifia. Anga ikavaa joho jeusi tititi kama kizimwili. Giza totoro likazagaa na kushamiri kote. Usiku mchanga ukashika hatamu na kutamalaki.

Mimi na umbu zangu tulijipweteka pwete makochini. Tulipiga soga na porojo huku mama na mnuna wangu Vumilia wakituandalia kilalio.

Muda mrefu haukupita kabla ya meza hazijachafuliwa kwa mapochopocho kochokocho. Harufu nzuri ya ruhani ilihinikiza kote sebuleni. Mara mchuano kati ya magego na mlo ukashika kasi. Kila mmoja wetu aliushtaki ubao kwa kukifanyia kilalio haki yake. Mara kunyofoa minofu nyofu nyofu, mara kutafuna chapati

tafutafu sikwambii kugwengwenya mifupa  
gwengwenyegwengwenye!

Naam, kumbe walikuwa wameona jingine wavyele wa  
zamu walipoamba mambo ni kangaja huenda yakaja!  
Ghafla bin vuu, kama ajali tuligutushwa na kishindo  
kikuu kilichotisha kama Izraili. Naam, baridi ina  
msisimo kwa kondoo mwenye manyoya haba. Sote,  
tulituama na kuachama. Tukabaki tumemaka,  
ungetuona ungedhani ni mahuluki waliotwangwa  
ghafla kwa barafu nyusoni.

Nilinyanyuka na kusimama dede huku nikitetemeka  
tetete kama kifaranga aliyenyeshewa na mvua ya  
gharika msimu wa kipupwe. Nililemewa na woga wa  
kunguru. Nao wasiwasi wa mwasi ukanivaa kama  
lebasi, japo kwa wayowayo na jakamoyo, niliyatia  
nyatunyatu kama lumbwi na kutupa jicho. Viwiliwili  
vya watu wenye kurunzi vilionekana vikikimbia  
mkikimkiki vingine kukurukakara kuelekea  
barabarani. Naam, kumbe ni kweli mbiu ya mgambo  
ikilia kuna jambo! Mara tepetepe na mipayuko kama  
ya wehu ikatamalaki na kuhinikiza hewani.

“Leta mitungi! Ondoka nichote! Umaskini kwaheri!  
Ondoa ushamba, bwege wewe! Kila mtu anataka

kuchota mafuta usilete ubaradhuli!” Ndizo sauti zilizowakosesha insi usingizi. Naam, aliye na macho haambiwi tazama, na fumbo mfumbie mjinga, mwerevu ataling’amua. Papo hapo, nikang’amua kuwa vya bwerere vilikuwa vimepatikana. Nikaghairi kubaki nyuma kama koti la mzee na kuamua kuwa mbele kama mfuko wa shati. Nani asiyejua kuwa aliye kando haangukiwi na mti na asiye kuwapo na lake halipo? Nilinyakua mtungi nyakunyaku na kufululiza kenyekenye hadi palipokuwa na umati wa watu. Nilipofika, watu walikuwa wakiangukiana. Wengine walifokeana ungedhani walikuwa na kamusi ya matusi vinywani. Lakini ng’o, walikuwa mwande. Kelele zao ziliangukia masikio yenye nta, yasiyosikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Naam, wahenga walilonga, kila mwamba ngoma huvuta kwake. Sikujali, sikubali togo wala jando. Nikasahau la wahenga kuwa asiyejali hupata ajali isiyojali wala kubali. Lakini ningekumbukaje ilhali kipendacho moyo ni dawa.

Tukiwa katika pilkapilka za kuyateka mafuta ya bwerere, jamaa fulani njorinjori, mrefu kama mlingoti na mweusi tititi kama lami akawasha sigara. Kabla

hata hajapuliza fundo la kwanza, mlipuko wa ajabu  
ulisikika. Naam, pafukapo moshi pana moto. Lo!  
Lahaula lakwata! Moto mkubwa ulizuka zu! Kama  
mizuka. Watu waliduwaa na kubung'aa ng'aa!  
Kukurukakara za kujinusuru zikashika kasi. Moto  
ukazidi kuenea na kurindima. Ikawa ni patashika,  
nguo kuchanika na miguu niponye. Watu  
wakagongana dafrau na kuangushana kama magari  
barasteni. Kila mmoja akajaribu kuisalimisha aushi  
yake. Moto nao ukaendelea kuwaka na kuchoma bila  
huruma. Maskini wanyonge walichomekana na  
kuteketea teketeke kiasi cha kutoweza kutambulika.  
Watu takriban hamsini walienda jongomeo na  
wengine kugeuzwa vilema. Niliponea katika tundu la  
sindano. Chapuchapu! Waama, tama mbele mauti  
nyuma. Naam, wahenga walisema ukupigao ndio  
ukufunzao. Maneno tama, pupa na papara nikayazika  
katika kaburi la sahou, maadamu, yanaweza kuwa  
chanzo cha baa, balaa bin beluwa. Tangu siku hiyo,  
maisha yangu yalichukua mkondo mpya.

--- Mwisho ---